**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NANGURUWE

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA**

**SHULE YA SEKONDARI YA NANGURUWE**

**S.L.P 129**
**MTWARA**

**NAMBA ZA SIMU**
**Mkuu wa Shule: 0656095634 au 0613 902 648**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0617 853 769**
**Mwalimu wa Malezi: 0675 374 143**

**TAREHE…………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………......................................................................**
**S.L.P ……………………………………....**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NANGURUWE ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA MKOANI MTWARA**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii na atasoma tahasusi ya ……………….

Shule ya Sekondari Nanguruwe ipo 32km kutoka Manispaa ya Mtwara Mikindani kwenye Barabara ya Newala katika kijiji cha Nanguruwe, kata ya Nanguruwe, Tarafa ya Ziwani Halmashauri ya ya Wilaya ya Mtwara. Usafiri wa basi kutoka mjini Mtwara unapatikana katika kituo cha mabasi Mkanaledi, nauli ni shilingi 2000 hadi Nanguruwe, na hapo utachukua pikipiki kwa shilingi 1000 hadi shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe …………… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………… Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………..

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

1. Mashati mawili meupe mikono mirefu aina ya tomato yenye ukubwa wa kutosha bila kuchomoka likichomekewa
2. Suruali nyeusi esteem namba 1 mbili (2) zenye malinda mawili, chini upana usiopungua inch 13 yenye turn up, isipite kisigino na isiwe ya kubana yenye mifuko mitatu.
3. Viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga na kamba (gidamu) nyenye visigino vifupi.
4. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali
5. Tai mbili zinapatikana shuleni kwa gharama
6. Sweater (Rangi ya Bluu) kwa ajili ya kipindi kifupi cha baridi wakati wa darasani.
7. Nguo za kushindia (shamba dress) suruali mbili rangi ya kijivu ziwe na turn up inayofunika soksi na upana inch 13 yenye marinda mawili na T-shirt mbili za round kola rangi ya zambarau (purple)
8. T-Shirt mbili za kola (form six) rangi ya Maroon (damu ya Mzee) zenye nembo ya shule. (zinapatikana maduka yaliyo Jirani na shule kwa gharama ya Tsh 15,000)

**NB**: NGUO ZA **NYUMBANI HAZIRUHUSIWI** NA MWANAFUNZI ANAPASWA KUVAA NGUO ZILIZOELEKEZWA TU**.**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari (counter book 4 **QUIRE**) 10
ii. Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika.
iii. Graph paper (vitabu viwili kwa mwaka), scientific calculator, dissection kit
iv. Godoro( ft 2½ x 6) inch 4
v. Nguo za michezo
vi. Shuka Jozi mbili rangi ya Bluu bahari.
vii. Foronya na taulo
viii. File moja la kutunzia mitihani
ix. Chandarua ft 2½ x 6 (Rangi nyeupe)
x. Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
xi. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
xii. Track Suit moja (1) ya michezo rangi ya dark Blue
xiii. Raba za michezo jozi mbili
xiv. Sanduku imara la kutunzia vifaa vyake (Tranka).
xv. Tochi ya kumsaidia wakati umeme unapokatika.
xvi. Nguo za ndani za kutosha na vifaa vya usafi
xvii. Rimu 2,
xviii. Sabuni ya kusafishia chooni Lt. 5. (*Halisi ya dukani*)
xix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, Fagio laini (Soft broom) moja (1) **AU** Fagio ya nje (chelewa) moja (1).
xviii. Mwanafunzi kama hana bima ya afya anatakiwa kuja na kiasi cha shilling 50,400 kwa ajili ya bima ya afya (NHIF)

### 2.3 Michango mbalimbali

Michango ifuatavyo anapaswa kuja nayo wakati wa kuripoti

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango inatakiwa ilipwe kupitia Benki ya NMB katika ACCOUNT **Na**. **70601200094** ya Nanguruwe Secondary School. Jina la akaunti **Nanguruwe Secondary REC/AC.** Pia uje na risiti halisi (Original) ya benki (Bank Pay In Slip) iliyoandikwa jina la mwanafunzi.

## 3.0. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kusema uongo.
v. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
vi. Kupiga au kupigana
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma

**Vifuatavyo viambatanishwe na fomu hii**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu, Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Vivuli vya vyeti vifuatavyo:- Cheti cha kuzaliwa, slip ya matokea ya mtihani wa kidato cha nne (Result slip) (kinapatikana shule aliyomaliza kidato cha nne)

**Tafadhali soma kwa makini maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**…………………………………………**

**HASSANI I. GOGOMEKO**

**Mkuu wa Shule**

## TAARIFA BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI

(Form hii ijazwe na irudishwe shuleni)

1. Jina la mwanafunzi.............................................................................. Kidato cha................................
2. Kabila la mwanafunzi...........................................................................................................................
3. (a) Tarehe ya kuzaliwa.......................................................................................................................

   (b) Wilaya alikozaliwa mwanafunzi..................................................................................................

   (c) Mkoa..................................................................................................................................
4. Dini ya mwanafunzi..........................................................................................................................
5. Tatizo la mwanafunzi kiafya..............................................................................................................
6. Tatizo la mwanafunzi kitabia..............................................................................................................
7. Jina kamili la baba............................................................................................................................

   Anuani kamili: .................................................................... Simu........................................................

   Kazi yake: ........................................................................................................................................
8. Jina kamili la mama.........................................................................................................................

   Anuani kamili: ............................................................... Simu..............................................................

   Kazi yake: ........................................................................................................................................
9. Jina kamili la mtu/mlezi anayemhudumia mwanafunzi ikiwemo kumpatia mahitaji yake muhimu;

   .................................................................................................................................................
10. Uhusiano wa mwanafunzi na mlezi..................................................................................................

    Anuani kamili.................................................................. Simu.........................................................

    Kazi yake; ...........................................................................Umri.......................................................
11. Baba na mama wanaishi pamoja / wametengana (kata isiyohusika)
12. Uwepo wa wazazi: Baba - YUPO/HAYUPO kama amefariki lini......................... Mama - YUPO/HAYUPO kama amefariki lini.................................................
13. Majina na picha za watu wasiozidi wanne watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa dharula au wito maalumu;-

    i. JINA: ........................................................................................
       SIMU: ........................................................................................
       UHUSIANO: ..........................................................................

    ii. JINA: ........................................................................................
        SIMU: ........................................................................................
        UHUSIANO: ..........................................................................

    iii. JINA: ........................................................................................

SIMU: ……………………………………………………………………………..

UHUSIANO: ………………………………………………………………

## FOMU YA MAKUBALIANO YA MZAZI / MLEZI

Mimi ........................................................................................................... ambaye ni mzazi / mlezi wa ......................................................................................................... aliyetoka shule ya sekondari ...................................................... Wilayani .........................................Mkoa wa …………................. nimesoma na nimeyaelewa maagizo ya kujiunga na shule hii

Na

Ninakubali au sikubali masharti yafuatayo

i. Nafasi aliyopewa kijana wangu kujiunga na kidato cha tano katika mwaka wa masomo 2026/2027
ii. Kijana wangu kufuata sheria, maagizo na masharti yote ya shule ya sekondari Nanguruwe
iii. Kulipa michango yote itakayoelekezwa na shule
iv. Kumpatia mwanangu mahitaji yote ya shule kama yalivyoorodheshwa na shule
v. Kufuatilia kwa karibu maendeleo ya kila siku ya mwanangu kitabia, mwenendo na taaluma.
vi. Kupokea taarifa zote kutoka shuleni zinazomuhusu mwanangu.

Sahihi...................................................................

Tarehe...................................................................

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ........................................................................................ wa kidato cha.....................................

Nimesoma na kuzielewa sheria za shule na naahidi kuzitii na kutimiza taratibu zote zilizowekwa.

Sahihi: .................................................................... Tarehe: .............................................................

# FOMU YA KUTOSHIRIKI MGOMO AU MAANDAMANO

JINA: …………………………………………………………………………………………………

SAHIHI: ………………………………. TAREHE: …………………………..

### MKATABA WA KUTOJIHUSISHA NA VURUGU, MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

*(Fomu hii ijazwe na mwanafunzi na kurudishwa shuleni)*

Mimi ……………………………………………ambae ni mwanafunzi wa kidato cha …………………. katika shule hii naahidi kutojihusisha kwa namna yoyote katika migomo, fujo au kosa lolote la jinai ambalo litahatalisha amani au litakalokuwa kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za shule.

Endapo ikithibitika kuwa nimetenda kosa au makosa tajwa hapo juu sitakuwa na pingamizi juu ya hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa dhidi yangu.

Jina la mwanfunzi ………………………………………………………………………………………

Sahihi ya mwanafunzi …………………………………………………………………………………

Tarehe ………………………………………………………………………………………………………

Jina la mzazi / mlezi ………………………………………………………………………………….

Sahihi ya mzazi / mlezi …………………………………………… Tarehe ……………………………

**MTWARA DISTRICT COUNCIL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

THE HEADMASTER

NANGURUWE SECONDARY SCHOOL,

S. L. P 129,

MTWARA

TO:

The Medical Officer

..........................................................
..........................................................
………………………………………

**RE: NAME.......................................................................................................................**

Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for full time course of Secondary Education at Mtwara Girls Secondary School.

1. Eye sight.......................................................................................................................
2. Hearing.........................................................................................................................
3. Speech..........................................................................................................................
4. Venereal Diseases.........................................................................................................
5. Neurosis........................................................................................................................
6. Pregnancy.....................................................................................................................
7. VDRL …………………………………………………………………………………
8. TB ……………………………………………………………………………………

Doctor's Remarks...............................................................................................................
.........................................................................................................................................
.........................................................................................................................................

Doctor's Advice...................................................................................................................
.........................................................................................................................................
.........................................................................................................................................

Doctor's Name....................................................................................................................

Signature............................................... Rubber Stamp ………………………………………..

Date...................................................................................................................................